**[Toleo la Mei 2015]**

# Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia:

# Kitabu cha Muongozo

**Kimetolewa na Kituo cha Ujamaa**

**Yaani *The Ujamaa Centre for Community Development & Research***

**(zamani kiliitwa *the Institute for the Study of the Bible & Worker Ministry Project*)**

**Sehemu ya 2:**

[Mifano ya Mitaala ya Biblia]

Mtaala wa Biblia wa 1 – Ukandamizaji wa kiuchumi Marko 12:41-44 56

Mtaala wa Biblia wa 2 – Ardhi & Usalama wa chakula Mathayo 6: 9-13 87

**Mtaala wa Biblia wa 1 – Ukandamizaji wa kiuchumi Marko 12:41-44**

Utangulizi

Tumeshazungumzia mtaaala wa Biblia kwa kina katika sura zilizopita; hapa tunajaribu kutoa mfano wa mtaala wa Biblia. Mtaala huu unahusu yanayowasibu wakristo wa kawaida wanaokandamizwa na kanisa kwa madai makubwa ya utoaji. Mfano huu unatumia mbinu ya majadiliano ya vikundi vidogo kwa kila swali na kisha kurudi katika kundi kubwa ili kutoa mrejesho.

Taarifa Muhimu kwa muwezeshaji

Mtaala huu wa Biblia upo kwenye kitabu cha muongozi sehemu ya 1. Huu ni Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia (MBMH). Kabla ya kuongoza mtaala huu yafaa usome maelezo ya utangulizi kutoka kwenye kitabu cha muongozo sehemu ya 1, na hasa sura ya 2 ambayo inahusu maandalizi ya mtaala wa Biblia na wajibu wa muwezeshaji wa mtaala wa Biblia (sura ya 3)

Hatua ya 1

Unaweza kuanza kwa kumkaribisha kila mmoja, na kufungua kwa maombi.

Hatua ya 2

Soma kifungu cha maandiko toka katika tafsiri ya Biblia inayotumika na washiriki wa warsha ya mtaala wa Biblia.

Muombe mshiriki mmojawapo kusoma kifungu, yafaa mtu anayesoma awe na sauti ya kutosha, yenye nguvu.

Kama washiriki wana Biblia zao basi msomaji anapoendelea kusoma na wao waendelee kufuatilia kifungu katika Biblia zao. Watie moyo washiriki kusikiliza kwa makini.

Hatua ya 3

Muulize kila mshiriki swali hili: Swali la 1. Kifungu kinahusu nini? Swali hili lijadiliwe na washiriki wote kama kundi moja. Andika majibu wanayotoa kwenye karatasi kubwa ya ukutani ili kila mtu aone jibu lake limeandikwa.

Jambo Jema la kufanya katika Hatua ya 3. Ni jambo jema kumuomba kila mshiriki ‘kunong’onezana’ na jirani yake jinsi anavyowaza kifungu kina maana gani. Kwa njia hii ya kuanzisha majadiliano kwa mtindo wa kila mtu ‘kunong’onezana’ na jirani yake, unakuwa umetengeneza mazingira ya uhuru kwa washiriki kuzungumza na kuvunja ukimya. Ingawa mtu anaweza kusita mwanzoni lakini kadri muda unavyoenda anajifunza kuwa siyo vibaya kuongea na mtu mwingine ndani ya ukumbi. Kwa njia hii unakuwa umetengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya mtaala wote.

Hatua ya 4

Wagawe washiriki katika vikundi vidogo. Yafaa kuwa na watu wanne hadi sita hivi katika kila kikundi. Kila kikundi yafaa kiwe na karatasi kubwa ya kuandika majibu yao, Biblia na peni au penseli.

Andika Swali la 2 kwenye karatasi kubwa ya ukutani. Swali lionekane wazi na kila mwanakikundi: Swali la 2 Soma Marko 12:38-40 (vifungu vinavyotangulia mistari ya 41-44). Je kuna uhusiano gani kati ya 12:41-44 na 12:38-40? Kama ndivyo, eleza uhusiano huo? Vikundi vijadili kila swali peke yake na kisha viandike majibu yake.

Hatua ya 5

Mwisho wa muda wa majadiliano, kila kikundi kisome muhtasari wake. Kisha vikundi vyote vikutane pamoja kama kundi moja. Andika taarifa ya kila kikundi katika karatasi kubwa na kuibandika ukutani ili kila mtu aweza kuona. Kama kuna muda wa kutosha washiriki wengine wanaweza kuongeza mawazo mengine waliyonayo kwenye taarifa nzima ya vikundi.

Hatua ya 6

Baada ya utoaji taarifa kwa pamoja, kila kikundi kirudi kwenye sehemu yake ya majadiliano.

Andika swali la 3 kwenye karatasi kubwa. Swali lionekane wazi na kila mwanakikundi.

Uliza Swali la 3 kama ifuatavyo: sasa someni Marko 13:1-2, kifungu kinachofuata mara baada ya Marko 12:41 – 44. Je kuna uhusiano gani kati ya 13:1-2 na 12:38-44? Kama ndivyo, eleza uhusiano huo? Vikundi vijadili swali na kuandika majibu.

Hatua ya 7

Vikundi virudi kwenye kundi kubwa na kutoa taarifa ya majadiliano. Yafaa vikundi vitoe taarifa kwa mtiririko tofauti. Kama mara ya kwanza ulianza na kikundi cha kwanza, sasa anza na cha pili au cha mwisho, nk. Andika majibu yako kwenye karatasi kubwa ili kila mtu ayaone.

Hatua ya 8

Baada ya kutoa taarifa vikundi vitarudi tena kwenye majadiliano. Andika swali la 4 kwenye karatasi kubwa na lionekane wazi na kila mtu.

Uliza swali: Swali la 4 Yesu aliingia hekaluni saa 5:27 na kuondoka saa 7:2 mchana. Katika sehemu hii ya kifungu:

Akina nani au makundi gani ni wahusika wakuu?

Je tunawafahamu

Wana uhusiano gani kati yao?

Chora picha ya uhusiano kati ya wahusika au makundi ya wahusika hekaluni. Mchoro wako unaeleza nini kuhusu mtiririko wa masimulizi kwa ujumla?

Kisha vikundi viende kwenye majadiliano na kuandika majibu yake.

Maelezo muhimu kwa muwezeshaji

Swali hili ni la kina na ni muhimu sana, hivyo yafaa utoe muda wa kutosha (kama dakika 30 – 45) na uwatie moyo wanavikundi kuchora picha au mchoro kwenye karatasi kubwa ya kuweka ukutani baada ya majadiliano yao.

Hatua ya 9

Tena, mwisho wa majadiliano, kila kikundi kisome muhtasari wa majadiliano yake ili kila mmoja ajue yaliyomo katika maelezo ya mjadala. Kila kikundi kiwasilishe kwenye kundi kubwa 'mchoro wa uhusiano' wa wahusika hekaluni.

Hatua ya 10

Yafaa utoe muhtasari wa majibu ya vikundi vyote kwa kutengeneza picha moja inayowasilisha picha zote kuhusu wahusika wa hekalu na mahusiano yao katika Marko 11:27-13:2. Unahitaji karatasi moja kubwa kwa ajili ya jambo hili. Wakati unafanya zoezi la kutengeneza picha moja, waombe washiriki kuendelea na majadiliano kila mtu na jirani yake.

Hatua ya 11

Baada ya utoaji wa taarifa washiriki wanapaswa warudi katika vikundi vyao.

Andika swali la 5 na 6 kwenye karatasi kubwa. Swali lionekane wazi na kila mshiriki.

Swali la 5 Utendaji wa hekalu la Yerusalem ulikuwaje wakati wa Yesu?

Swali la 6 Kama Marko angepaswa kutuma ujumbe mfupi wa simu ya kiganjani, yaani SMS kuhusiana na sehemu hii ya maandiko, angesemaje?

Vikundi vijadili maswali haya.

Hatua ya 12

Baada ya kurudi kwenye kundi kubwa na kutoa taarifa ya Swali la 5 na 6, washiriki watapaswa warudi tena kwenye vikundi vyao vidogo

Andika swali la 7 na 8 kwenye karatasi kubwa. Weka karatasi mahali ambapo swali litasomeka wazi na kila mtu.

Swali la 7 Swala hili linatupa ujumbe gani katika mazingira yetu?

Swali la 8 Ni mpangokazi gani tunaweza kuuweka ili kutekeleza mtaala huu wa Biblia?

Vikundi viende vijadili maswali haya.

Hatua ya 13

Vikundi vitoe taarifa kwa kila mtu kuhusu majadiliano yao na mpangokazi wao. Yafaa vikundi vitoe taarifa kwa mtiririko tofauti kila vinaporudi kutoa taarifa. Tena andika majibu yao kwenye karatasi kubwa ya kubandika ukutani au ubaoni, ili kila mtu aweze kuona na kujifunza kutoka mpangokazi wa wengine.

Hatua ya 14 Hitimisha mtaala wa Biblia. Unaweza kuhitimisha mtaala wa Biblia kwa sala, na kumuomba Mungu amuwezeshe kila mmoja aliyeshiriki kutekeleza mpangokazi wake.

**Mtaala wa Biblia wa 4 – Ardhi & Usalama wa chakula Mathayo 6: 9-13 87**

Utangulizi

Mtaala huu wa Biblia unahusu mambo ya ardhi, pia ni mtaala wenye unauhusiano na mada ya 10, 11 na 12 katika kitabu cha muongozo sehemu ya 1. Ni mfululizo wa mitaala ya Biblia inayoandaliwa na Kituo cha Ujamaa kwa kushirikiana na shirika la Mpango wa Ardhi katika Kanisa, lenye lengo la kuwezesha watu kumiliki ardhi katika vijiji vyao katika nchi ya Afrika Kusini.

Maelezo muhimu kwa muwezeshaji

Mtaala huu wa Biblia upo kwenye kitabu cha muongozi sehemu ya 1. Huu ni Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia (MBMH). Kabla ya kuongoza mtaala huu yafaa usome maelezo ya utangulizi kutoka kwenye kitabu cha muongozo sehemu ya 1, na hasa sura ya 2 ambayo inahusu maandalizi ya mtaala wa Biblia na wajibu wa muwezeshaji wa mtaala wa Biblia (sura ya 3)

Hatua ya 1

Unaweza kuanza kwa kumkaribisha kila mmoja, na kufungua kwa maombi.

Hatua ya 2

Soma kifungu cha maandiko toka katika tafsiri ya Biblia inayotumika na washiriki wa warsha ya mtaala wa Biblia.

Muombe mshiriki mmojawapo kusoma kifungu, yafaa mtu anayesoma awe na sauti ya kutosha, yenye nguvu.

Kama washiriki wana Biblia zao basi msomaji anapoendelea kusoma na wao waendelee kufuatilia kifungu katika Biblia zao. Watie moyo washiriki kusikiliza kwa makini.

Hatua ya 3

Muulize kila mshiriki swali hili: Swali la 1. Kifungu kinahusu nini? Swali hili lijadiliwe na washiriki wote katika kundi moja. Andika majibu wanayotoa kwenye karatasi kubwa ya ukutani ili kila mtu aone jibu lake limeandikwa.

Jambo Jema la kufanya katika Hatua ya 3. Ni jambo jema kumuomba kila mshiriki ‘kunong’onezana’ na jirani yake jinsi anavyowaza kifungu kina maana gani. Kwa njia hii ya kuanzisha majadiliano kwa mtindo wa kila mtu ‘kunong’onezana’ na jirani yake, unakuwa umetengeneza mazingira ya uhuru kwa washiriki kuzungumza na kuvunja ukimya. ingawa mtu anaweza kusita mwanzoni lakini kadri muda unavyoenda anajifunza kuwa siyo vibaya kuongea na mtu mwingine ndani ya ukumbi. Kwa njia hii unakuwa umetengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya mtaala wote.

Neno Uhakika wa Chakula lina maana gani? Uhakika wa Chakula ni hali ya kuwa na hakika ya uwepo wa chakula muhimu kwa matumizi ya binadamu. Ni uhakika kwamba kutakuwa na chakula cha kutosha wakati wote.

Wazo Jema: mara nyingi tumeizoea mno Sala ya Bwana kiasi kwamba tunashindwa kuona na kuelewa ina maana gani. Ili kuwasaidia washiriki kuwaza kwa kina kuhusu kifungu na jinsi kinavyohusiana na maisha yao, muombe kila mmoja atulie kimya kabisa kwa muda, na awaze kwamba hajawahi kamwe kusikia sala kama hii. Kila mtu awaze kana kwamba Sala ya Bwana ndiyo anaisikia kwa mara ya kwanza, na kila mmoja ajaribu kuitazama sala hii kwa 'macho mapya'.

Hatua ya 4

Wagawe washiriki katika vikundi vidogo. Yafaa kuwa na watu wanne hadi sita hivi katika kila kikundi. Kila kikundi yafaa kiwe na karatasi kubwa ya kuandika majibu yao, Biblia na peni au penseli.

Andika Swali la 2, 3, 4 na 5 kwenye karatasi kubwa ili kila mshiriki aweze kuona kwa urahisi. Kila kikundi kijadili maswali, kuandika muhtasari wa majadiliano kwa kila swali kwenye karatasi kubwa waliyopewa.

Swali la 2 Kwa kuzingatia Sala ya Bwana kama ilivyoandikwa katika Mathayo, Ufalme wake Mungu "uje" wapi?

Swali la 3 Mistari ya 11 Na 12 inauelezaje ufalme wa Mungu?

Swali la 4 Kwa nini Yesu anajali sana kuwa na "riziki ya kila siku" (mstari 11)? Je unakumbuka mistari yoyote katika Biblia ambapo Yesu anaonyesha kujali swala la chakula?

Swali la 5 Kwa nini Yesu anazungumzia "[ma]deni" yetu (mstari 12)? Unakumbuka mistari mingine ambapo Yesu anazungumzia madeni na madhara ya madeni?

Hatua ya 5

Vikundi vitoe taarifa ya majadiliano yao kwenye kundi kubwa ili kila mshiriki asikie. Ili kuokoa muda vikundi vitoe taarifa ya swali moja moja kwa zamu ili majibu yanayofanana yasirudiwe kutolewa taarifa.

Hatua ya 6

Andika Swali la 5, 6, 7, 8 na 9 kwenye karatasi kubwa. Maswali yaonekane wazi kwa kila mshiriki. Vikundi vijadili na kujibu maswali. Majibu yaandikwe kwenye karatasi kubwa watakazopewa.

Swali la 5 Ni nani katika mazingira yako unayoishi anauhitaji wa "riziki ya kila siku"? Kwa nini?

Swali la 6 Ni akina nani katika mazingira unayoishi wanahitaji kusamehewa "[ma]deni" yao? Kwa nini?

Swali la 7 Ufalme wa Mungu unaweza kuwa na maana gani mahali unapoishi hasa kwa watu ambao wanahitaji riziki ya kila siku na kusamehewa madeni yao? Je, kutatokea mabadiliko gani kwao, likifanyika linalopaswa kufanyika?

Swali la 8 Ni “majaribu” na “maovu” gani (mstari 11) yanaweza kutuzuia kujenga ufalme wa Mungu hapa duniani?

Swali la 9 Utafanya nini ili kuhakikisha uwepo wa ufalme wa Mungu hapa duniani? Andika orodha ya mambo unayoweza kufanya, au mpangokazi utakao utekeleza.

Hatua ya 7

Kwa mara nyingine tena, baada ya muda wa majadiliano, kila kikundi kitoe taarifa kwenye kundi kubwa.

Hatua ya 8

Hitimisha mtaala wa Biblia. Kwa kuwa sasa kila mmoja ana ufahamu mpya kuhusu uhakika wa chakula, unaweza kuhitimisha warsha kwa kuwaongoza wote katika Sala ya Bwana, na kumuomba Mungu kuwawezesha wote waliyoshiriki kuuleta ufalme wa Mungu duniani.

Kanuni za Ufafanuzi

Kifungu hiki kimezoeleka sana, na kama ilivyo kwa vifungu vingine, kimeshatawaliwa. Hatuzingatii mafundisho yake ya kina. Tunadhani tunajua maelezo yana maana gani. Mtaala huu wa Biblia umeandaliwa katika namna inayomuwezesha mshiriki kuona kuwa kifungu hiki siyo cha kawaida, yaani kilichozoeleka tu; mtaala unamuwezesha mshiriki kusikia sauti ya maandiko kwa upya! Tunaposoma kwa uangalifu tunagundua jinsi Yesu alivyojihusisha na mahitaji ya kila siku ya watu maskini na waliosahaulika, na hawa walikuwa ndiyo wafuasi wake wa kwanza. Sala ya Bwana iliyopo katika kitabu cha Mathayo inatuwezesha kuona jinsi Sala ya Bwana ilivyokuwa ni sala ya watu maskini, kabla haijafanywa kuwa sala ya watu wenye kipato katika kanisa (tazama sala hii katika Luka).

Yamkini sala hii ilihusiana na matatizo ya ardhi, hususani jinsi watu waliyo katika mazingira magumu walivyopoteza ardhi yao. Jinsi kitabu cha Samweli kinavyokosoa utawala wa kifalme katika 1 Samweli 8, inaonyesha madhara yaliyowapata watu baada ya ardhi yao kuchukuliwa na mfalme. Matokeo yake ni utumwa! Wengi wao waliyomfuata Yesu yamkini walipoteza ardhi na mali zao kutokana na mfumo wa utawala wa hekalu (unaoelezwa katika kitabu cha Samweli na kukosolewa na Yesu pia katika Marko 11 na 12 – tazama mfano wa mada ya mtaala katika kitabu cha muongozo sehemu ya 1 ukurasa wa 23-27). Yesu anatambua kuwa kwa sababu wamepoteza ardhi yao, wanauhitaji wa riziki ya kila siku. Na zaidi, baada ya kupoteza ardhi yao kutokana na madeni, njia pekee ya kuwawezesha kurejeshewa ardhi yao ni kusamehewa madeni yao. Hata hivyo, Yesu anajua kuna majaribu na maovu mengi yanayozuia ufalme wa Mungu usidhihirika hapa duniani, kama ulivyo mbinguni. Tumepoteza nguvu ya sala hii kwa sababu tumeshindwa kuisikiliza kwa makini; tumeikariri na tunaikiri lakini jambo la ajabu ‘hatuisikii’ sauti yake!